

Thamani Ya Utii
(The Value of Obedience)

Na

Terry Warford

Thamani Ya Utii

Na

Terry Warford

Novemba 12, 2011

Thamani Ya Utii

Mara nyingi sisi katika Kanisa la Kristo tunashutumiwa kwa kuwa makini katika kufuata neno la Mungu. Tunashutumiwa kwa kuwa na imani kali, kijadi, au neno linalopendwa ni “uhalali”.

Hivyo ili kulinda imani yetu, ebu tuangalie thamani ya utii. Tutaona kwamba kuna thamani hasili katika kufuata neno la Mungu kwa karibu kadiri tuwezavyo. Tutapata kwamba utii siyo uhalalisho, lakini kimsingi kuonyesha vitu vyote vya roho ambavyo tunavikosa.

Kwanza kabisa, tunaona kwamba utii ni unyenyekevu. Tunaponyenyekea kwa kulitii neno la Mungu, tunafuata mfano wa Yesu Kristo mwenyewe. Fil. 2:8, *“Tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.”* Angalia Yesu alijinyenyekeza na akawa mtii. Ni mfano ulioje kwetu sisi kuufuata. Msitari wa 5, *“Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo pia ilikuwa ndani ya Kristo Yesu,”* Utii ni unyenyekevu, siyo uhalalisho..

Utii ni njia moja wapo tunayomsifu Mungu. Tunamsifu Mungu kwa njia nyingi, kama vile katika nyimbo, maombi, kutangaza jina lake katika ulimwengu. Pia tunamsifu Mungu kwa kumtii. Zab. 148:7-8, *“Msifuni BWANA kutoka nchi, enyi nyangumi na vilindi vyote. Moto na mvua yam awe, theluji na mvuke, upepo wa dhoruba ulitendao neno lake.”* Vitu hivi vya asili vilikuwa vinamsifuje Mungu? Kwa kulitimiza neno lake. Tena, mfano ulio mkuu kwetu kuufuata katika Zaburi 112:1, *“Haleluya, heri mtu yule amchaye BWANA, apandezwaye sana na maagizo yake.”* Utii ni mfumo wa kusifu, siyo kienyeji.

Utii ni matokeo ya imani. Katika sura ya 11 ya Waebrania, sura kuu juu ya imani, kila mfano unaotolewa unawaonyesha watu wakimtii Mungu kupitia imani yao. Siyo mmoja kutokutii kwa imani. Hakuna aliyefanya “bure” kwa imani. Walifanya kile alichowataka Mungu kufanya kwa imani. Tusome mistari ya 7-8, *“Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari ya mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu aliunda safina apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani. Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi, akatoka asijue aendako.”* Kwa imani Nuhu aliandaa, kwa imani Ibrahimu alitii. Na imani inatoka wapi? Rum. 10:17, *“Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.”* Siyo kwa kubadilisha neno lake. Hatuwi makini kwa kutii; bali tunakuwa waaminifu.

Utii ni njia pekee katika amani. Efe. 4:3, “*Na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani.*” Tunafanyaje hivyo? Kwa kusikiliza na kumtii Roho. Ufu. 3:22, “*Yeye aliye na sikio na alisikie na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*” Roho aliwavuvia mitume, (Mdo 1:2), walioandika chini maagizo ya Bwana kwetu sisi, (2 Pet. 3:1-2). Kutii neno la mitume ni njia ya kwenda katika amani. 2 Pet. 1:2, “*Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu.*”

Mwisho, utii ni jinsi tunavyomwonyesha Mungu tunavyompenda. 2 Yohana 6, “*Na huu ndio upendo tuenende kwa kuzifuata amri zake. Hii ndio ile amri kama mlivyosikia tangu mwanzo kwamba mwenende katika hiyo.*” Yoh. 15:9-10, “*Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu, kama vile mimi nilivyoizishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.*”

Hivyo utii sio utii wa kukosa ukweli, vitu vya roho vya shauku. Utii ni unyenyekevu, sifa, imani na amani. Kutii sio unyenyekevu. Utii ni upendo.

Rum. 6:17, “*Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake.*”

Katika Jina la Yesu,
Terry Warford

